

**MAKUBALIANO YA KUKABIDHI MTOTO KWA MTU MCHANGA NA ONDOLEO LA DHIMA –
Mtumizi wa Basi la NASHVILLE**

Tafadhali soma kwa umakini kabla ya kuweka sahihi.

Ikiwa mtoto (watoto) wako atatumia usafiri wa basi kwenda na kutoka shuleni, familia yako pia itapaswa kufanya maamuzi ya namna mtoto (watoto) wako atafika na kuondoka kwenye kituo cha basi kilichopangwa. Ikiwa utapenda mtoto (watoto) wako aweze kutembea kutoka kituo cha basi kwenda nyumbani huku akisindikizwa na mtu mwenye **umri kati ya miaka 11 na 18 (“Mtu Mchanga”)**, utapaswa kumaliza kujaza hati hii kwanza na kukubali kufuata masharti yote yaliyomo ndani yake.

Tafadhali zingatia kwamba unaweza pia kuwa na chaguo la kumruhusu mtoto (watoto) wako kutembea kutoka kituo cha basi kwenda nyumbani bila kusindikizwa na mtu mzima au mtu mchanga. Hata hivyo, ikiwa hivyo, bado utatakiwa kumaliza kujaza hati tofauti, inayoitwa, **Hati ya Mtumizi wa Basi** ya Rocketship.

Taarifa ya Mtu Mchanga

Ninaelewa na kukubali kwamba nimempa ruhusa mtu mchanga aliyeorodheshwa hapa chini, ambaye **ana umri wa kati ya miaka 11 na 18 (“Mtu Mchanga”)**, kumchukua mtoto (watoto) wangu kutoka kituo chake/chao cha basi kilichopangwa.

Jina la Mtu Mchanga (La Kwanza & La Mwisho):

Tarehe ya Kuzaliwa ya Mtu Mchanga: _____

Darasa la Mtu Mchanga: _____

Uhusiano baina ya Mtu Mchanga na Mtoto (Watoto) wangu:

**Ongeza nyongeza ya Watu Wachanga hapa chini, ukihitaji.*

Taarifa za Mwanafunzi wa Rocketship

Nimempa ruhusa Mtu (Watu) Mchanga aliyeorodheshwa kwenye fomu hii kumchukua mtoto (watoto) afuataye, **ambaye mimi ni mzazi/mlezi halali kwake**, kutoka kwenye kituo chao/chake cha basi kilichopangwa.

Jina la Mtoto: _____ Tarehe ya Kuzaliwa:
_____ Darasa: _____

Jina la Mtoto: _____ Tarehe ya Kuzaliwa:
_____ Darasa: _____

**Ongeza nyongeza ya watoto hapa chini, ukihitaji.*

Ninaelewa na kukubali kwamba Mtu (Watu) Mchanga PEKEE aliyeorodheshwa katika fomu hii ndiye atakaeruhusiwa kumchukua mtoto (watoto) aliyeorodheshwa kwenye fomu hii.

Ninaelewa kwamba, kwa madhumuni ya hati hii, “nyumbani” ina maanisha anuani ya nyumba ambayo nimetoa kwa Rocketship kama sehemu ya nakala zangu za usajili, au mahali pa kituo cha mtoa huduma ya matunzo baada ya shule, ambacho nimekitoa kwa Rocketship.

Ikiwa Mtu Mchanga rasmi hatokuwepo kwenye kituo cha basi pindi basi litakapofika kwa ajili ya kushusha, Ninaelewa kwamba mtoto (watoto) wangu atarudishwa shuleni isipokuwa pale patakapokuwa na mtu mzima mwenye umri zaidi ya miaka 18 kwenye kituo cha basi atakaemsindikiza mtoto (watoto) wangu kwenda nyumbani.

Ninaelewa kwamba mtoto (watoto) wangu hatoruhusiwa kutembea kwenda nyumbani akiwa na mtu mwenye umri wa chini ya miaka 18 ambaye hajaorodheshwa kwenye fomu hii.

Ninaelewa na kukubali kuitaarifu shule upesi kama, katika wakati wowote, Nitataka kuongeza au kuondoa mtoto, ambaye mimi ni mzazi/mlezi halali kwake, kuingia au kutoka kwenye hati hii.

Ninaelewa na kukubali kuitaarifu shule upesi kama, katika wakati wowote, Nitataka kuongeza au kuondoa Mtu Mchanga kuingia au kutoka kwenye hati hii.

Ninaelewa na kukubali kwamba Rocketship **haina wajibu wa kufuatilia tabia za wanafunzi** mara baada ya kutoka kwenye basi, hii ni pamoja na kipindi cha kutembea kutoka kituo cha basi kwenda nyumbani.

Ninatambua na kukubali hatari zozote na zote kwa mtoto (watoto) wangu zitakazotokana na kutembea kutoka kituo cha basi kwenda nyumbani bila ya uangalizi wa mtu mzima. Kwa kuzingatia ruhusa ya mtoto (watoto) wangu kutembea kutoka kituo cha basi kwenda nyumbani bila kusindikizwa na mtu mzima, Ninaachilia, naondoa, na kuweka usalama kwa dereva wa basi, mtoa huduma ya usafiri, pamoja na Shule za Umma za Rocketship na Bodi yake ya Wakurugenzi, maofisa, waajiriwa, watoa huduma ya kujitolea, wakala, wadhamini, wadau au wajumbe kutoka dhima

yoyote na zote kwangu, mtoto (watoto) wangu, mwakilishi wetu binafsi, wajumbe, na ndugu wa karibu, za majeraha yoyote na yote, madai, madhara, haki za kuchukua hatua au sababu za kuchukua hatua, ambazo Mimi au mtoto (watoto) wangu anaweza kuwa nazo au kupata, kutokana na mtoto (watoto) wangu kutembea kutoka kituo cha basi kwenda nyumbani bila ya kusindikizwa na mtu mzima.

Kwa umakini nimesoma makubaliano haya na nimeelewa maudhui yake. Ninatambua kuwa hii ni hati na ondoleo la dhima, na kwa hiari Ninaweka sahihi.

Ichapishwe na Mzazi/Mlezi

Jina _____

Anuani _____

Namba za Simu _____

SAHIHI _____ Tarehe: _____